HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

Mhe. Mwenyekiti,
Wahe. Wajumbe,
Baraza la Madiwani.

YAH: RASIMU YA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

1.0. UTANGULIZI

Mhe. Mwenyekiti,
Uwasilishaji wa Rasimu ya mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni:-

i. Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022

ii. Mapitio ya Mpango na Bajeti wa mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia mwezi Disemba 2022 na

iii. Rasimu ya Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024

1.1. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mhe. Mwenyekiti,
Jedwali lifuatalo linaonyesha bajeti ya mapato ya Halmashauri na Mgawanyo wa kila chanzo:-

Na	Chanzo cha Mapato	Makisio ya Mwaka 2021/2022	Jumla ya kilichopokelewa Julai, 2021 - Juni 2022	% ya mwaka
1	Vyanzo vya Ndani	5,306,258,756.00	5,539,797,762.55	104
2	Ruzuku PE	32,831,658,000.00	35,652,734,172.00	108
3	Mapato Mengineyo- OC	2,416,708,736.48	2,204,389,788.68	91
4	Miradi ya Maendeleo	14,637,871,224.17	11,066,624,142.17	76
Jumla Kuu		**55,192,496,716.65**	**54,463,545,865.4**	**98**

1.2. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA HALMASHAURI KWA MWAKA 2021/2022

Mhe. Mwenyekiti,

Katika kutekeleza mpango wa bajeti ya mwaka 2021/2022, Halmasahuri imepata mafanikio na changamoto kadhaa ambazo zimeongeza ufanisi/ubunifu katika utendaji kazi na kutoa huduma bora za Kijamii na Kiuchumi kwa Wananchi. Baadhi ya mafanikio na changamoto ni kama ifuatavyo:-

1.2.1. MAFANIKIO

i. Ujenzi wa vyumba 55 vya madarasa kupitia fedha za UVIKO 19 katika Shule 20 za Sekondari ambapo vyumba vyote vimekamilika na vinaendelea kutumika.
ii. Halmashauri imefanikiwa kuendesha zoezi la uwekaji wa anuani za Makazi kwa maeneo yote ndani ya Halmashauri.
iii. Halmashauri imefanikiwa kuwapandisha vyeo jumla ya Watumishi 348, Watumishi 131 wamebadishiwa vyeo na jumla ya Watumishi 33 waliajiriwa.
iv. Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi 3 (3 in 1) katika Kituo cha Afya Kyimo ambapo ujenzi umekamilika na nyumba ipo tayari kwa matumizi.
v. Ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa dharura (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu, ujenzi umekamilika na jengo lipo tayari kuanza kutumika.
vi. Ujenzi wa miundombinu ya Maji katika Shule 2 za Msingi za Bugoba na Ikukisya pamoja na Shule ya Sekondari Kisondela ambapo ujenzi umekamilika na kuanza kutoa huduma.
vii. Ujenzi wa Bweni katika shule ya Msingi Katumba II ambapo ujenzi umefikia asilimia 75.
viii. Ujenzi wa Kituo cha Afya Ndanto, Iponjola, Kinyala na Kyimo ambapo vituo hivyo vipo hatua mbalimbali za ukamilishaji.
ix. Ukamilishaji wa zahanati mbili za Isyonje na Ilenge ambazo zipo katika hatua ya ukamilishaji pamoja na ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika zahanati ya Simike na Kyobo ambazo zipo katika hatua za umaliziaji.
x. Ujenzi wa jengo la ghorofa moja (OPD na Wodi ya Wanaume na Wanawake) katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 45 pamoja na

ukarabati wa Jengo la Magonjwa ya kuambukizwa ‘’isolation ward’’ ambalo utekelezaji wake umefikia asilimia 95

xi. Ufanisi wa utoaji wa Chanjo za aina zote ikiwa ni pamoja na chanjo ya UVIKO 19 kwa ufanisi wa zaidi ya asilimia 99.

xii. Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa na jengo la Utawala katika shule ya Msingi Katumba II pamoja na ujenzi wa vyumba 02 vya madarasa na matundu 06 ya vyoo katika Shule ya Msingi Lutete ambapo miundombinu yote imekamilika na kuanza kutumika.

xiii. Halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo yenye jumla ya kiasi cha Shs.**732,027,500.00** kwa vikundi **69** vinavyoendeleza shughuli za viwanda vidogo vidogo, ufugaji na kilimo ambapo vikundi vya wanawake **43**, vijana vikundi **23** na watu wenye ulemavu 03. Aidha Kikundi kimoja kimefanikiwa kuanzisha kiwanda kidogo cha kufyatua tofali, kingine utengenezaji wa chaki, viwili vya uselemala na ufundi uashi, usindikaji wa mazao ya maziwa, mazao ya viungo, na mafundi cherehani”. Kati ya fedha hizo. Mchango wa Halmashauri ni Tsh. 321,107,740 ambayo ni sawa na na asilimia 101.88 ya lengo la Tsh.315,194,548 na kiasi cha Tsh. 410,919,760.00 inatokana na Marejesho ya vikundi.

xiv. Uzalishaji wa mazao ya biashara hususan zao la kahawa uliongezeka kutoka tani 685 kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia tani 1,302 mwaka 2021/2022.

xv. Bei ya zao la kahawa iliongezeka kutoka wastani wa Sh 3,500.00 kwa kilo msimu wa mwaka 2020/2021 hadi kufikia wastani wa tsh 6,750 kwa kilo msimu wa mwaka 2021/2022.

xvi. Kupanda kwa ufaulu kwa Wanafunzi wa Kidato cha Nne kutoka asilimia 93.57 mwaka 2020 hadi asilimia 94.2 mwaka 2021 na kwa kidato cha sita ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 99.62 mwaka 2021 hadi asilimia 99.82 mwaka 2022. Na kwa upande wa Elimu ya msingi, ufaulu uliongezeka kutoka asilimia 90.59 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 93.2 mwaka 2022

xvii. Ufunguzi wa shule 02 za Sekondari ya Kyobo Kata ya Ikuti na Kikota Kata ya Kiwira.

xviii. Jumla ya Wakulima 30,824 walisajiliwa katika mfumo na wanaendelea kununua Mbolea kwa Mawakala kwa bei elekezi.

xix. Halmashauri imefanikiwa kukusanya mapato ya ndani jumla ya shilingi **5,539,797,762.55** sawa na asillimia 104% ya lengo la kukusanya kiasi cha shilingi **5,306,258,756.00**

xx. Jumla ya Tshs. 1,198,825,934 ziliweza kutolewa kwa walengwa wa kaya maskini zinazohudumiwa na TASAF ambapo jumla ya kaya 5,552 za walengwa zilinufaika.

xxi. Jumla ya miti 1,598,300 kati ya miti 1,500,0000.00 ya aina mbalimbali(matunda, kivuli ,mbao) imepandwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe katika taasisi za umma, mashamba binafsi ya taasisi na watu binafsi.

1.2.2. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2021/2022

i. Ikama ya Watumishi kuwa ndogo ukilinganishwa na idadi ya watumishi iliyopo. Ikama ya Watumishi inayohitajika ni 3,930, waliopo ni 3,201 na hivyo kuwa na upungufu wa Watumishi 729

ii. Vyombo vya usafiri (Magari) vinavyotumika na vya muda mrefu na hivyo kuhitaji marekebisho ya mara kwa mara.

iii. Uhaba wa Masoko ya mazao ya Kilimo na Mifugo hali inayopelekea mazao hayo kuuzwa kwa bei ndogo ukilinganisha na gharama halisi za uzalishaj**i**

iv. Kutokuwepo kwa masoko ya uhakika kwenye mazao ya mifugo hasa Kwenye zao la ngozi na uwepo wa bei ndogo kwa zao la maziwa ukilinganisha na gharama za uendeshaji.

v. Baadhi ya Wanavikundi kutorejesha mikopo yao kwa kuzingatia kanuni, taratibu na mikataba yao ambapo hadi Juni 2021, kiasi kilichorejeshwa ni Tsh: 315,660,500.00 kati ya Tsh: 350,400,000.00.

vi. Kushuka bei ya mazao hasa wakati wa mavuno ya msimu mkubwa, hii inapelekea kushuka kwa kipato kinachotokana na mazao hayo wakati mwingine gharama za uzalishaji hazirudi, hivyo kufanya wakulima wavunjike moyo kuendelea kuzalisha mazao kwa tija.

vii. Kuchelewa kwa fedha za Wahisani kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbai kwa wakati.

viii. Miche ya miti inayozalishwa kutotosheleza mahitaji yaliyopo kutokana na ufinyu wa bajeti

1.2.3. UTATUZI WA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

i. Halmashauri kuomba vibali vya ajira mpya ili kupunguza changamoto ya upungufu wa Watumishi uliopo.

ii. Halmashauri kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya magari yaliyopo ili yaendelee kutoa huduma

iii. Kwa msimu wa 2022/2023 Serikali imeweka ruzuku kwenye pembejeo hususan mbolea hali iliyosaidia bei ya mbolea kushuka kutoka tsh 140,000.00 msimu wa 2021/2022 mpaka tsh 70,000.00 kwa msimu wa 2022/23.

iv. Halmashauri kuendelea kushawishi wawekezaji mbalimbali kwenye viwanda vya maziwa ili kuweza kuboresha soko la maziwa wilayani na kuwezesha vikundi vitakavyokuwa vinatengeneza bidhaa za ngozi.

v. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kutengeneza mazingira mazuri ya masoko ya mazao ya wakulima kama vile ujenzi wa maghala baridi ya kuhifadhi mazao ya mbogamboga na matunda, kuanzisha masoko zaidi kwenye kata na vijiji, kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji na wanunuzi kutoka nje ya Wilaya na nje ya nchi.

vi. Kuboresha mfumo wa uhakiki na uchambuzi wa Vikundi vinavyokidhi vigezo vya kukopeshwa ambapo imeundwa Timu maalum inayojumuisha Wataalam mbalimbali kufanya uchambuzi wa Vikundi ikiwemo matumizi sahihi ya mfumo wa TPLMIS. Pia Halmashauri imechukua hatua za kisheria kwa Vikundi sugu ambavyo havikurejesha mikopo yao licha ya juhudi kubwa iliyofanyika ya kuvifuatilia. Hadi sasa kuna Vikundi viwili vimefikishwa mahakamani. Aidha tunaendelea kutoa elimu kwa vikundi kuhusu kufanya marejesho kwa wakati kwa kuzingatia mikataba.

vii. Halmashauri kwa kushirikiana na taasisi zingine za Serikali kuendelea kutenga bajeti itakayotosheleza uandaaji wa vitalu vya miiche ili kuongeza zaidi kiwango cha upandaji miti.

viii. Halamashauri kuendelea kuwakumbusha Wahisani na Wadau wengine wa Maendeleo kutoa fedha kwa wakati ili kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa mujibu wa bajeti.

2.0. MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI WA MWAKA WA FEDHA 2022/23 HADI KUFIKIA MWEZI DISEMBA 2022.

Mhe. Mwenyekiti,

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha **57,812,357,000.00.** Hadi kufikia mwezi Disemba 2022, Halmashauri imepokea kiasi cha Shs. **25,772,390,108.88** sawa na asilimia **44.5** ya makisio yote .

NA	Chanzo cha Mapato	Makisio ya mwaka 2022/2023	Jumla ya kilichopokelewa Julai- Disemba 2022	% Julai - Desemba 2022
1.	Vyanzo vya ndani	6,131,460,000.00	3,093,348,914.77	50.45
2.	Ruzuku PE	40,209,676,00.00	18,617,730,062.00	46.3
3.	Mapato mengineyo - Oc	1,186,569,000.00	557,581,625.00	47
4.	Miradi ya Maendeleo	10,284,652,000.00	3,503,729,507.11	34
	Jumla kuu	**57,812,357,000.00**	**25,772,390,108.88**	**44.5**

Mhe. Mwenyekiti,

Hadi kufikia mwezi Disemba 2022, Halmashauri imetumia jumla ya **Tsh 23,751,887,018.38 s**awa na asilimia **92** ya fedha zilizopokelewa.

NA	Chanzo cha Mapato	Jumla ya kilichopokelewa Julai- Disemba 2022	Jumla ya Matumizi Julai- Disemba 2022	% ya nusu mwaka
1.	Vyanzo vya ndani	3,093,348,914.77	2,971,064,406.75	48.5
2.	Ruzuku PE	18,617,730,062.00	18,617,730,062.00	46.3
3.	Mapato mengineyo - Oc	557,581,625.00	281,578,720.63	50.5
4.	Miradi ya Maendeleo	3,503,729,507.11	1,881,513,829.00	53.7
	Jumla kuu	**25,772,390,108.88**	**23,751,887,018.38**	**92.1**

Mhe. Mwenyekiti,

Halmashauri imeendelea kutekeleza miradi kulingana na mapokezi ya fedha za miradi hiyo, Pia Halmashauri imeendelea kusimamia miradi iliyotolewa fedha mwaka 2021/2022 na utekelezaji wake kuvuka mwaka. Aidha, Halmashauri imeendelea

kuwasiliana na wadau wa maendeleo ili kuchangia miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Halmashauri.

2.1. MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA UTATUZI WA CHANGAMOTO HIZO KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 HADI DISEMBA 2022

2.1.1. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 HADI DISEMBA 2022

i. Halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya tshs. 132,000,000.00 kwa vikundi 8, vikiwemo vikundi 7 vya Wanawake pamoja na Kikundi 1 cha Watu wenye Ulemavu kupitia mfumo mpya wa TPLMIS. Kwa kipindi hicho Halmashauri imeweza kuchagia kiasi cha Tshs. 105,000,000.00 kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kutokana na mapato yake ya ndani.

ii. Halmashauri imefanikiwa kujenga vyumba vya madarasa 10 kupitia fedha kutoka Serikali kuu (kiasi cha shilingi 200,000,000.00) kwa ajili ya mapokezi ya kidato cha kwanza 2023 katika shule za sekondari Ziwa ngosi, Kyobo, Isaka, Igogwe,Nkunga, Kibisi, Kayuki na Ndembela One.

iii. Halmashauri imefanikiwa kujenga mabweni mawili katika shule ya Sekondari Kisondela kupitia fedha kutoka Serikali kuu ambapo utekelezaji wa mabweni yote mawili umefikia asilimia 75.

iv. Halmashauri imefanikiwa kupima vipande 16,650 katika vijiji vilivyofanyiwa Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi, utolewaji wa Hati 46 maeneo ya mjini na hati za kimila 92.

v. Halmashauri imefanikiwa kuanzisha kampuni tanzu ambayo ikianza kufanya kazi faida yake itaongeza Mapato ya ndani ya Halmashauri

2.1.2. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 KWA KIPINDI CHA JULAI - DISEMBA 2022.

i. Uhaba wa Watumishi kutokana na watumishi kustaafu/kufariki/kuhama kwa sababu maalumu. Ikama ya Watumishi inayohitajika ni 3,930, waliopo ni 3,201 na hivyo kuwa na upungufu wa Watumishi 729

ii. Bado suala la ukomo wa bajeti (ceiling) ya fedha za mitihani linaendelea kuathiri ufanyikaji wa Mitihani ya Kuhitimu Elimu ya Msingi na Darasa la Nne.

iii. Uwepo wa vifo vya Mama Wajawazito imeendelea kuwa changamoto katika Halmashauri yetu pamoja na mafanikio yaliyipatikana

2.1.3. MIKAKATI ILIYOPO YA KUKABILIANA NA BAADHI YA CHANGAMOTO ZILIZOAINISHWA.

i. Halmashauri kuendelea kuwasilisha maombi ya ajira za watumishi mbalimbali kulingana na upungufu uliopo. Aidha Halmashauri kufanya mabadiliko ya Muundo wa ajira kwa Watumishi (‘Recategorization’) kulingana na alichosomea Mtumishi husika.

ii. Halmashauri kuwasiliana na Ofisi ya Rais **TAMISEMI** kuomba kutengeneza ukomo vifungu vya bajeti ya Mitihani ili kuendana na uhalisia kiutendaji.

iii. Halmashauri inaendelea kuongeza juhudi za kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa akina mama Wajawazito kuhudhuria kliniki mara wanapojitambua kuwa Wajawazito ili kupunguza hatari za vifo.

3.0. RASIMU YA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

Mhe. Mwenyekiti,

Rasimu hii imezingatia mambo mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi wa mwaka 2020.

ii. Mafanikio na changamoto za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022 na Bajeti ya mwaka 2022/2023 hadi kufikia Disemba, 2022

iii. Miradi iliyoibuliwa na Wanachi kwa mfumo wa Fursa na Vikwazo ulioboreshwa (Improved O&OD)

iv. Viwango vya Ukomo wa Bajeti (Budget Ceiling) zilizotumika katika mwaka 2022/2023 kwakuwa hadi sasa viwango vipya vya ukomo wa Bajeti havijatolewa.

v. Mpango Mkakati wa Halmashauri wa Miaka Mitano 2020/2021 - 2025/2026

3.1. MAPENDEKEZO YA RASIMU YA MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MPANGO WA UTEKELEZAJI NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

Mhe. Mwenyekiti,

Naomba kuwasilisha rasimu ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa ajili ya kupata maoni, ushauri na mapendekezo kabla ya kuwasilisha katika ngazi nyingine kama utaratibu unavyotaka.

3.2. VIPAUMBELE VYA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

i. Kuimarisha makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha usimamizi wa makusanyo ya mapato katika vyanzo vilivyopo ili kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi;

ii. Kuboresha miundombinu ya Biashara na Masoko ili kujenga mazingira mazuri ya Biashara na ukusanyaji wa mapato

iii. Kuboresha Miundombinu ya Elimu na Afya

iv. Kuboresha mazingira ya uwekezaji Wilayani kwa kuboresha miundombinu ya uwekezaji pamoja na kuendeleza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji ili kukuza uchumi wa jamii pamoja na kuwashirikisha wadau wa ndani na nje wa Halmashauri.

v. Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi.

vi. Kununua lori kwa ajiri ya kusomba taka na shughuli za miradi ya maendeleo.

3.3. UMBILE LA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri inategemea kukusanya na kutumia kiasi cha Tsh. **58,197,398,459.00** kwa mchanganuo ufuatao:-

NA.	RUZUKU	ENEO LA UTEKELEZAJI		KIASI
1	Ruzuku kutoka Serikali Kuu	a.	Mishahara	**40,209,676,000.00**
		b.	Matumizi mengineyo	1,162,341,000.00
JUMLA NDOGO				**41,372,017,000**
2	Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	a.	Fedha za ndani	4,934,048,500
		b.	Fedha za nje	5,102,938,000
JUMLA NDOGO				**10,036,986,500.00**
3	Mapato ya ndani (Own source proper)	a.	Matumizi mengineyo	2,169,399,686.40
		b.	Miradi ya maendeleo	1,446,266,457.60
JUMLA NDOGO				**3,615,666,144.00**

NA.	RUZUKU	ENEO LA UTEKELEZAJI		KIASI
4	Michango ya Elimu na Afya (Own Source others)	a.	CHF	87,094,367.00
		b.	NHIF	541,338,388.00
		c.	PAPO KWA PAPO	336,196,060.00
		d.	Ada na Michango ya Elimu	2,000,000,000.00
		e	Michango ya Kijamii	208,100,000.00
JUMLA NDOGO				**3,172,728,815.00**
JUMLA KUU				**58,197,398,459.00**

Aidha, Halmashauri inategemea kukusanya na kutumia kiasi cha Tsh **58,197,398,459.00**kwa mchanganuo ufuatao:-

A. MAPATO

Na.	Chanzo Cha Mapato	Kiasi
1	Serikali Kuu	46,306,065,500.00
2	Mapato ya Ndani	6,788,394,959.00
3	Wahisani	5,102,938,000.00
JUMLA		**58,197,398,459.00**

B. MATUMIZI

Na.	Aina ya Matumizi	Kiasi
1	Mishahara	40,209,676,000.00
2	Matumizi ya Kawaida	6,504,469,501.40
3	Miradi ya Maendeleo	11,483,252,957.60
JUMLA		**58,197,398,459.00**

Mhe. Mwenyekiti

Kutokana na mchanganuo wa Makisio ya mapato hapo juu, Halmashauri ina uwezo wa kuchangia asilimia **11.66** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Mhe. Mwenyekiti,

Maelezo ya kina ya mapato na matumizi yanaelezwa katika viambatisho vifuatavyo:-

1. **Kiambata Na 1**

   Maoni ya Kamati mbalimbali zilizopitia na kujadili rasimu ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024

2. **Kiambata Na 2**

   2A Mchanganuo wa mapato ya ndani kwa kila chanzo

   2B Mchanganuo wa mapato ya ndani kwa kila Kata

3. **Kiambata Na. 3**

   3A Mapendekezo ya ukomo wa matumizi ya kawaida kwa mapato ya ndani

   3B Mchanganuo wa matumizi ya Kawaida wa Mapato ya ndani kwa kila Idara

   3C Mapendekezo ya ukomo wa matumizi ya kawaida kwa Ruzuku kutoka Serikali Kuu

   3D Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida wa Ruzuku kutoka Serikali kuu

   3E Mapendekezo ya ukomo wa matumizi ya bajeti ya Mapato lindwa

   3F Mchanganuo wa matumizi ya mapato lindwa ya Afya

4. **Kiambata Na 4**

   4A Mapendekezo ya ukomo wa matumizi ya miradi ya Maendeleo kwa Mapato ya Ndani

   4B Mchanganuo wa miradi ya maendeleo kwa kila idara kupitia Mapato ya Ndani

   4C Mapendekezo ya ukomo wa matumizi ya miradi ya Maendeleo kwa Ruzuku kutoka Serikali Kuu

   4D Mapendekezo ya miradi ya Maendeleo itakayotekelezwa kupitia Ruzuku kutoka Serikali kuu.

5. **Kiambata Na 5**

   5A Mapendekezo ya ukomo wa matumizi ya fedha za Wahisani

   5B Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha za Wahisani.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha taarifa hii pamoja na viambata vyake:-

Noah Sikwese
KNY: MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
RUNGWE